# Piga Hatua Maishani

## Toleo la Watoto




Na Elmer H. Murdoch

# Neno Muhimu kuhusu Kutumia Kijitabu Hiki

Wapendwa watoto: Wavulana na Wasichana

Ninaandika kukusaidia kuelewa makusudio ya kijitabu hiki. Kitakueleza jinsi ulivyo wa thamani kwa Kristo na namna ambavyo anataka umjue Yeye kama unavyo mjua rafiki wako. Hii itatokea utakapojua kumwamini na kumtumainia Yeye. Kijitabu hiki kitakuonyesha jinsi ya kufanya hivyo. Najua wengi wenu tayari mnafahamu Yesu na mnaweza hata kunukuu aya za Biblia. Jambo hilo ni la maana sana. Lakini, hiyo si kusema umeokoka hadi Kristo abadili matendo na mitazamo yenu.

Ninajua wengi wenu hufanya mambo ili kuwapendeza wazazi, waalimu, na wengine mnaowapenda. Lakini usimkaribishe Yesu katika maisha yako ili kumfurahisha mtu fulani, au kabla hujawa tayari. Atakuja katika maisha yako kama unataka afanye hivyo, na kama wewe unafanya hivyo ili kumfurahisha Yeye.

Mara utakapoelewa vyema jinsi ya kuokolewa, basi ni wakati wa maana sana, kwa sababu sasa unaweza kutubu - badilika kutoka kutenda maovu - na uamini - jipeane katika Bwana Yesu. Uamuzi huu utaathiri maisha yako sasa na kama utaenda Mbinguni.

Katika kitabu hiki utakuta ngazi. Kila "hatua" ya hiyo ngazi inawakilisha kiwango tofauti cha kujifunza njia za kumjua Bwana Yesu kibinafsi. Unapoamua kuwa umesimama juu ya "hatua" ipi, kwa kweli huna budi kuitafakari!

Baadhi yenu mnajua bila shaka ya kwamba Yesu yuko. Alikusaidia kuona dhambi zako ambazo zilikuwa

baya na labda ulilia kwa sababu ya dhambi hizo zako. Huyu ndiye Yesu anayekuita ili utubu na umwamini Yeye. Je, umefanya hivyo? Ikiwa bado, Mungu anangojea ili umwalike Yeye moyoni mwako. Kisha Yeye ataleta mabadiliko katika maisha yako.

Unaweza kupanda ngazi hii kwa haraka kiasi unachoelewa na uko tayari kumfanya Kristo achukue nafasi ya kwanza katika maisha yako. Kiasi cha muda kinachotumika kinategemeana na wewe mwenyewe. Usichelewe, lakini usijiweke katika "hatua" yoyote ambayo hujaifikia bado.

Baadhi ya watoto ni wema na watiifu lakini wengine ni watukutu sana. Kristo alikufa kwa ajili ya wote kwa kuwa hakuna aliye mwema na kuweza kwenda mbinguni yeye mwenyewe. Warumi 3:10. Unaposoma kijitabu hiki mara kwa mara kitakuwa kama mwanga ambao unaangaza zaidi na zaidi na utaelewa nini maana ya kuwa Mkristo wa kweli.

Neno moja la mwisho. Tunaweza kuwaelezea jinsi ya kuokoka. Ni Mungu tu anayeweza kukuambia kuwa umeokoka. Kristo kupitia Roho Wake hufanya hivyo. Warumi 8:16 inasema, "Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu."

Mtu yeyote anapojikabidhi kabisa kwa Kristo watajisikia tofauti kwa dhambi na mitazamo yao isiyo sahihi na watataka kumfurahisha Kristo. Kumbuka wewe na watu wa familia yako mnaweza kuokolewa kadiri kila mmoja anavyotubu na kuamini. Haya ni mapenzi ya Mungu kwa wao na kwako. Mungu anakupenda zaidi ya ninavyo weza kukueleza.

Sasa, soma kijitabu hiki na ugundue hatua ambayo wewe upo juu yake.

Elmer H. Murdoch

## Je, unadhani Nani...

- aliumba ulimwengu wako?
- anatoa uhai kwa mimea na wanyama?
- anajua kila kitu unachofanya na kusema?
- kweli ana kuthamini WEWE?

# *MUNGU!*

*"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi."*

**Mwanzo 1:1**

***Mungu alimtuma mwanaye Yesu duniani ili wewe upate kujifunza jinsi Mungu alivyo. Yesu anaweza kufanya hivi kwa sababu Yeye yu sawa na Mungu.***

## *Yesu kweli ni...*

**MWEMA** - Hajakosea jambo lolote. Hata kidogo!


**HEKIMA** - Anafahamu lipi ni jema na lipi ni baya. Anaweza kukuonyesha kwa nini unahitaji kufanya uamuzi sahihi.

**HURUMA** - Anaweza kusaheme kukosea kwako.

Ndiyo maana kila mvulana na msichana anapaswa kuvutwa na Yesu Kristo.

*Nukuu zote za Maandiko Matakatifu katika kijitabu hiki kidogo ni kutoka katika Biblia Takatifu.*


Yawezekana umetingwa mno na mambo mengine kiasi cha kushindwa kufikiri juu ya Mungu na Mwanawe, Yesu Kristo.



## Kutaka kufahamu juu ya Yesu Kristo ni kama kupanda ngazi. Kila hatua inakupeleka karibu zaidi na kule unakokusudia kwenda.


Unapopanda ngazi hizi utajifunza kuhusu ule upendo wa Mungu Baba na Yesu Kristo kwako.

**Baada ya hatua hizi kufafanuliwa, hebu eleza kwamba upo katika hatua ipi.**



*"Uzielekeze hatua zangu kwa neno lako…"*


**Zaburi 119:133**



# Hatua 1 - SIJALI

**Unaweza kufahamu mambo mengi juu ya Yesu na namna ya kuokolewa au ukawa unafahamu kidogo sana. Jambo la msingi ni kwamba kwa hakika hujali.**

WEWE, je?



*“Sisi, je! Tutapataje kupona,*
*tusipojali wokovu*
*mkuu namna hii?”*

**Waebrania 2:3**




Je, UPO katika hatua hii?

# Hatua 2 – NINAVUTIWA


## Baadhi  ya watu wanaposikia habari za Yesu Kristo na upendo Wake, hutaka kujua zaidi.

Je, WEWE unavutiwa kujua zaidi?



*"Nanyi mtanitafuta,*
*na kuniona, mtakaponitafuta*
*kwa moyo wenu wote."*

**Yeremia 29:13**



Je, WEWE upo katika hatua hii?

# Hatua 3 - NINASUTWA

## Hali hii hutokea pale unapofanya jambo baya na linakusuta.

Unaweza kuwa mvulana au msichana mwema kulinganisha na watoto wengine unaowafahamu. Lakini Mungu ametoa mtihani wa Wema, Amri Kumi, ili kujipima kama unafaa kuweza kuingia mbinguni. **Je, wewe u mwema kiasi hicho?**

### AMRI KUMI

1. **Usiwe na miungu mingine ila mimi**
2. **Usijifanyie sanamu ya kuchonga**
   *Je, huwa unajali kwanza wanaserere, wanyama au marafiki katika maisha yako?*
3. **Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako**
   *Taja jina la Mungu na Yesu Kristo wakati ule tu unapozungumza juu yao au unaposali.*
4. **Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase**
   *Siku moja katika saba tunaweza kutenga muda maalumu kwa ajili ya Bwana. Muda wetu wote, hata hivyo, ni wa Bwana.*
5. **Waheshimu baba yako na mama yako**
   *Wakati wote wasikilize na kuwatii wazazi wako, labda kama ni kwa jambo la dhambi.*
6. **Usiue**
   *Usiwadhuru watu au kuwa na chuki binafsi.*
7. **Usizini**
   *Usiguse mwili wa yeyote mahali ambapo hutakiwi. Tunza pendo lako kwa atakaye kuwa mume au mke wako.*
8. **Usiibe**
   *Usichukue kisicho kuwa mali yako.*
9. **Usimshuhudie jirani yako uongo**
   *Wakati wote sema ukweli.*
10. **Usitamani nyumba ya jirani yako**
    *Usiwe na wivu kwa vile walivyonavyo wengine.*

*Kutoka 20:3-17*

# Mtihani wa Mungu wa Wema

Amri Kumi za Mungu

Kufaulu ni 100%




Je, **daima** umemfurahisha Mungu katika njia **zote** hizi?

## Hatua 3 - NINASUTWA (inaendelea)

Hali ya kutompenda Mungu huitwa dhambi. Dhambi pia ni uamuzi wa kufuata njia zako mwenyewe japokuwa ni kosa.

Je, umewahi kutenda dhambi?

☐ NDIYO ☐ HAPANA

Hauko peke yako. **Biblia** inasema kwamba **WOTE** wamefanya dhambi na kutenda makosa! *Warumi 3:23*. Bwana Yesu anajua yote ufanyayo, hata kama rafiki zako na wazazi wako hawafahamu. Na, hata wakati ambapo hukamatwi!

Je, unakereka unapofanya makosa?


☐ NDIYO ☐ HAPANA

Kwa kiasi gani?

☐ Kidogo ☐ Sana ☐ Kiasi cha kunifanya nitake kubadilika

*"…Ee Mungu wangu, nimetahayari,naona haya kuinua uso wangu mbele zako, kwa maana maovu yetu ni mengi…"*


**Ezra 9:6**




*Je, UPO katika hatua hii?*
*HALI YA KUSUTWA INAWEZA KUSABABISHA…*

# Hatua 4 - NIKO TAYARI KUTUBU

## Toba ni kugeuka kutoka katika njia yako mwenyewe na kuelekea katika njia ya Yesu.



Kutaka njia yako mwenyewe ni ubinafsi. Maamuzi ya ubinafsi ni msingi wa dhambi zote.

Maamuzi ya kichoyo ni yale ya "mimi kwanza"-


- yanamhuzunisha Mungu na mwanaye Yesu Kristo
- yanasababisha matatizo kwako na kwa wengine.
- yanakufanya ujisikie vibaya.

Toba ni-

- kutojiweka mbele katika maisha yako ila Yesu tu.
- kutotaka kufanya dhambi tena.

*"…bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu."*

**Matendo 17:30b**




*Je, UPO katika hatua hii?*

*TOBA HUSABABISHA…*

# Hatua 5 - NINAAMINI

**Kuamini ni kujikabidhi kabisa kwa Bwana Yesu Kristo ili Yeye awe namba 1 katika maisha yako. Mungu amekuumba ili uishi na kumpendeza yeye.**

Ni kama kuingia katika mashua. Unapoingia katika mashua unakuwa na imani nayo kwamba hutaangamia kwa kufa maji.

Unapojikabidhi kwa Yesu usifanye hivyo ili …

- kumfurahisha mama au baba yako.
- kumfurahisha mwalimu wako, rafiki yako, au mchugaji wako.

Unapaswa kufanya hivyo ili …

- kuwapendeza Mungu na Yesu peke yao.
- kwa kuwa ni hakika unataka kufanya hivyo.
- kubadili maisha yako na dhambi zako kusamehewa.

Bwana Yesu alikufa msalabani kama adhabu kwa ajili ya dhambi zako na Mungu Baba yetu alimfanya kuwa hai tena. Sasa yu hai na anakusubiri wewe umpe nafasi ya kuwa Nahodha wa maisha yako.




*Kujitoa wewe mwenyewe kwa Yesu ni hatua ya imani.*

Zungumza na Bwana Yesu sasa. Taja dhambi zako. Mwambie Yeye kwamba unatubu na kuwa hutaki tena kurudia dhambi zako. Unasikitika sana kwa dhambi hizo. Kisha muombe akusamehe.

*"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."*

**I Yohana 1:9**

Biblia inasema kwamba Yesu mwenyewe atakuja kuishi ndani yako ukimwamini Yeye. Anakupa uzima wa milele - kwa sababu uzima wa milele uko ndani yake. Anaishi ndani yako na kukupa mema Yake.

*"…Mungu alitupa uzima wa milele; na uzima huu umo katika Mwanawe."*

**I Yohana 5:11**

Sasa mwombe Bwana Yesu Kristo aje maishani mwako kukuokoa ili WEWE uwe sehemu ya familia Yake.

Wakati utakapokuwa umemuamini Yeye na kumpokea, utajua. Atakueleza katika moyo wako.


*"Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wanawe, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu…"*

**Wagalatia 4:6**

Mshukuru Yeye kwa kufa kwa ajili yako.

*"Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka…"*

**Matendo 16:31**




Je, UPO katika hatua hii?

Mtu yeyote - mvulana au msichana - ampokeaye Kristo kama Bwana na Mwokozi -wanazaliwa katika familia ya Mungu kama ulivyozaliwa katika familia yako ya kibinadamu.

*"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu…"*

**Yohana 1:12**

Wakati Bwana Yesu atakapokuja katika maisha yako, uta…

- jua kwamba anaishi ndani yako.
- jua kwamba unakwenda mbinguni.

Na utaanza kumpendeza Bwana kwa…

- kumtii baba na mama.
- kuwa mwema kwa kila mtu.
- kufanya uamuzi sahihi.
- kusema ukweli.
- kuwa na hamu ya habari za Biblia.

**Namna hii ndiyo kuishi njia ya MUNGU!**

*"…basi chagua uzima, ili uwe hai wewe na uzao wako kumpenda BWANA Mungu wako…"*

**Kumbukumbu la Torati 30:19, 20**


# Kukusaidia kukua kama Mkristo:

1. Soma Biblia yako. (Toleo la watoto linaweza kusaidia)

2. Omba kwa Mungu Baba katika jina la Yesu kila siku. Mwambie Yeye shida zako na omba akusaidie.

3. Nenda kwenya kanisa ambalo watu hufundishwa Biblia.

4. Shirikisha rafiki zako yale ambayo Yesu amekufanyia na kile Anachotaka awafanyie.



*Kwa kuagiza nakala zaidi za kijitabu hiki wasiliana na:*
**Cistern Materials Translation & Publishing Center,**
P.O.Box 7576-00100, Nairobi, KENYA
Barua Pepe: info@cisternmaterialscenter.com
Simu: (+254) (0) 721330253 / 724780807
Tovuti: www.cisternmaterialscenter.com

Au wasiliana na:
sutlmail@aol.com; Tovuti:www.stepuptolife.com